



**REPUBLIC OF KENYA**  
**COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI**  
**SECOND ASSEMBLY –THIRD SESSION**

**THE HANSARD**

**Tuesday, 27<sup>th</sup> August 2019**

*The House met at the County Assembly Chamber,  
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

*[The Temporary Speaker (Hon. Mumba) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Good morning hon. Members, welcome to this morning's sitting. Kindly pass the microphone to the Chairperson of the Implementation Committee .

**NOTICE OF MOTION**

ADOPTION OF THE REPORT ON IMPLEMENTATION STATUS OF THE PETITION ON EMPLOYMENT  
DISCRIMINATION AGAINST THE LESS PRIVILEGED RESIDENTS

**Hon. Maitha:** Thank you Mr. Speaker. I rise to give a Notice of Motion. Pursuant to Standing Order No. 45 (1), I wish to give a Notice of Motion:-

THAT, this House adopts the Report of the Implementation Committee on the implementation status of the Report of Sectoral Committee on Administration, Labour and Social Services on the Petition made to the County Assembly on employment discrimination against the less privileged residents by the Department of Health and County Public Service Board laid on the Table this honourable House on Monday, 26<sup>th</sup> August 2019.

Thank you, Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you Chairperson. Next Order!

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

**MOTION**ADOPTION OF THE REPORT ON IMPLEMENTATION STATUS  
ON SHORTAGE OF ECD CAREGIVERS

**Hon. Maitha:** Thank you Mr. Speaker, I wish to move a Motion that this House adopts the Report of the Implementation Committee on the implementation status of resolution of the Report of the Sectoral Committee on Pre-primary Education, Vocational Training Motion on shortage of ECD caregivers laid on the Table of this House on 6<sup>th</sup> August, 2019.

Before I call upon hon. Mwambire to Second, allow me to give my submissions Mr. Speaker.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Hon. Mwambire.

*(Hon. Mwambire seconded)*

**Hon. Maitha:** Mr. Speaker...

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): No, Chairperson kindly take a seat first. You have moved a Motion and if you wanted to make your contribution, then you could have gone ahead and made your contribution even before you called the seconder to second the Motion. Now the fact that the seconder has gone ahead and seconded the Motion, I will give you an opportunity to give your remarks but as for now kindly hold your horses. Thank you Chairperson.

*(Question proposed)*

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): So, Chairperson would you wish to make your remarks now or you will give your remarks later.

*(Hon. Ziro stood on a Point of Order)*

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Yes what is your Point of Order?

**Hon. Ziro:** Thank you Mr. Speaker for this chance. The tradition of this House is to have the Order of Business for the week read before Business commences. However, the order of business has not been read so Members are not able to know what is coming after this. I have a prayer that we do have the Order of Business read before we can proceed but I seek your guidance. Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you Member for Garashi your concern has been noted. Usually the Business for the House is read on Mondays but it was not done yesterday but I want to assure you that the House Business Committee will convene after this and they will give us a supplementary Order Paper on the same; thank you. Chairperson of the Implementation Committee, you can make your remarks.

**Hon. Maitha:** Thank you Mr. Speaker. Allow me to give my submission before my seconder and the Members debate. The Committee on Implementation is mandated to scrutinize the resolutions of this House. We had a chance to call the CECM (County Executive Committee Member) Education and ICT and had a lengthy discussion and after that we had some findings. We saw as a Committee that the pace of implementations of the resolutions of this House was

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

too slow. We also noted that the Response of the CEC Education and ICT had no timelines; there was a difference in the number of caregivers.

The number of caregivers indicated was 334 but after scrutiny we realized that there were eight caregivers who were not posted and could not justify as to why they were not posted to their working stations. We made recommendations that where there is need for more caregivers they had to fill the eight positions before they add because we found out the number of caregivers is low per the number of ECD centres we have in Kilifi County. So, I urge this House to adopt this Report so that the Department can work on the eight and more caregivers to be employed. We also looked at the projects and their status was also wanting. The Response from the CEC was not satisfactory although some areas were handled well.

The CEC told us that contractors were not complaining and what we found is that contractors were complaining and since financial year 2014 to date, there are some projects which have stalled and if the CEC was honest that the contractors were not complaining, why were there stalled projects? Again, most of the contractors were not following the BQs (Bills of quantities). In our recommendations we stated that when this Report is adopted, the CEC will carry out a survey on the number of caregivers in schools and make sure that the stalled projects are completed in this financial year.

Mr. Speaker, I urge this House to adopt this Report so that we can have a clear roadmap on the implementation of the projects. We found that there is no good relationship between the community and the contractors. A contractor goes to the site without the community being informed, but when the CEC was asked this question, he tried to evade it saying they engaged the BOMs (Boards of Management) and that the contractors are working well with the BOMs. When this Report is adopted we have recommended that the contractors to work hand-in-hand with the Board of Management of the schools and in consultation with the office of the MCA in that ward so that we can have a good working harmony between the contractors, the community and the area Member of County Assembly (MCA).

In our findings, we found that most of the contractors are not using the BQ and this happened in...

*(Hon. Maitha spoke off record)*

...to give a few examples like the Matolani-Kikwanguloni in Ganze and a good number of projects that the contractors were not following the BQs. It is upon us to adopt this Report to make sure that the stalled projects are completed, the number of caregivers increased and the working relationship between the contractors, community and the MCA of that ward can be harmonized. I urge hon. Members of this House to adopt this Report so that we can push the Executive to do a good job for our people in the county. Thank you Mr. Speaker.

## COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR

### SYSTEM FAILURE

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you Chairperson and before the Members make their contribution on the same, I wish to communicate that the system is not in order. Whenever you wish to make a submission, kindly raise your hand and once you catch the Speaker's eye, I will give you the airtime for you to raise your concerns. Thank you.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

## CLARITY IN MEMBERS' SUBMISSION

I also want to add something on what you have just brought to the House and for the purpose of the Members to get convinced and support your Report. When you say contractors are complaining and they are not going by the BQs while the CEC says otherwise, I thought it would be wise if you could highlight to Members what the complaints were about. If they do not go by the BQs, what are they using because you are the ones who went to get the findings; with that, you can at least convince the Members to adopt this Report. Yes Chairperson Implementation.

**Hon. Maitha:** Thank you, Mr. Speaker. The point I was trying to drive here is that during our engagement with the CEC, he said that the contractors are not complaining because payment is done, but as we engaged further, we found that their projects have stalled since 2014 and the explanation of the CEC was that some of these projects were shelved because Ganze and Magarini had hunger; that is why the money was shifted from projects to attend to the hunger issue in Ganze and Magarini Sub-County.

How do you tell a Committee that a project was shaved because of hunger since 2014? In the financial year 2015/2016 and 2016/2017 the same project had not been implemented. Does it mean Ganze and Magarini still had hunger issues? This was a way where the CEC was escaping the reality. That is why I say the contractors down their tools because they had not been paid. Why does the CECM say that the contractors are not complaining? Members of the County Assembly from the wards, we know what is happening down there. As we engaged the CEC further, we came to realize that some contractors were forced to use sub-standard materials to complete this project because their payment was not done in time that is why I said the CEC was trying to evade reality.

Why am I saying that they are not using the BQs? Because it is known that the recommended roofing materials is coloured box profile but if you see their Report like the Matolani ECD they used the normal iron sheets. So, if the iron sheets used were contrary to the ones in the BQs, we are worried of the other materials used like the metals used during constructions, mostly they are covered with cement how do you tell if they used the right materials? That is why I am saying after the adoption of this Report, there should be a monitoring and evaluation Committee in conjunction with the works officer so that we can monitor and evaluate each and every step of a project. Mr. Speaker, I believe I have made this point clear to Members so that they can support and adopt this Motion.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you, Mr. Chairperson.

**Hon. Mwambire:** Thank you Mr. Speaker. I want to take this opportunity to thank my able Chairperson of the Committee on Implementation for giving us enough time to deliberate on the issues of implementation on this Department of Education and ECDE caregivers. I am supporting the adoption of this Motion. As a Committee, we had enough time to engage on the issues that my able Chairperson has raised. Let me also congratulate the Chairperson for Education for coming up with these findings which we deliberated on.

ECD education has been emphasized since devolution and according to the Report we had, some of the projects were not done to completion and according to the recommendation, I urge this House to adopt because this one will be an instrumental measure which will enable the Department to strengthen its belt over implementation of the projects.

I do not want to go back to the findings as highlighted by the Chairperson because I understand that every Member has the document. We came up with forceful recommendations that if this House adopts this Motion, then the Department will have to see that whatever we

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

agreed upon shall have to be done. We have seen some of the ECDE Centres were not done up to standard or even completed. We recommended that by the end of this financial year, all those projects should be completed.

Regarding the ECDE teachers, we found that there is a deficit of eight ECDE caregivers as per the earlier budgetary allocations. We urge the Department through the adoption of this document that those eight caregivers be replaced with immediate effect as stipulated in these recommendations per the Committee. With that, I would also urge hon. Members to adopt this Motion to give way for the CECM Education to act as per the recommendations. Thank you Mr. Speaker, Sir.

**Hon. Kenga:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Nitaanza kwa kusema kwamba naunga mkono kwa dhati Hoja hii iliyoletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji. Nampongeza na natambua juhudi zake pamoja na Kamati nzima kwa kuweza kumakinika kikazi, kuwajibika na kuhakikisha ya kwamba wanaweza kwa sasa kuleta Ripoti nyingi ambazo zitasaidia kuinua na kukuza kazi za Idara mbali mbali ndani ya Kaunti ya Kilifi.

Nitasema kwamba maswala mengi ambayo yamezungumziwa na Kamati hii ni mambo ambayo tumeyashuhudia kwa miaka mingi sasa. Ni aibu wakati serikali ya Kaunti inazindua mradi na wakati ule ule kuna shirika lisilokuwa la serikali linazindua mradi sehemu moja; mradi wa madarasa ya chekechea na mradi wa madarasa ambayo yanazinduliwa na shirika lisilokuwa la serikali. Mfano ni World Vision, Action Aid na mashirika mengine ambayo yanafanya kazi katika Kaunti ya Kilifi.

Wakati tumeenda kuzindua mradi, tunaelezea wananchi kwamba mradi huu madarasa haya mawili yanastahili kukamilika kwa siku tisaini (90); hiyo ni miezi mitatu, na mwanakandarasi amepewa wiki mbili akusanye vifaa vinavyotumika katika maswala ya ujenzi ili kazi ianze. Miaka miwili baadaye ule mradi wa serikali na ni madarasa mawili; hii miradi ambayo tunaizingumzia, hutaenda kuona mradi ambao umeanza na umechelewa ambao labda ni madarasa sita kwa pamoja, sana sana ni madarasa mawili na yakizidi labda manne. Lakini haya serikali imekosa kuwajibika kuyatekeleza kwa ule mda unaofaa ilhali yale mashirika kwa ule mda ambao jamii umepeana wanakuwa na nafasi nzuri ya kukamilisha ule mradi kwa ule mda unaofaa. Sasa tunapolinganishwa sisi kama serikali pamoja na mashirika inaonekana utendakazi wa serikali uko duni na mashirika yanafanya kazi vizuri na usimamizi wao uko bora zaidi.

Tunashangaa na kuulizana hii changamoto ni vipi tutaithibiti na kwa nini tuweze kuendelea kwa maswala yale? Tulipokaa na kujadili mambo ya ADP, mambo ya *the County Fiscal Strategy Paper*, tuliweza kukubaliana na tukasema ni jukumu la seriklai kuajiri waalimu wa chekechea. Wakati Gavana wetu anasukumia elimu isiyo na malipo, na pia ya lazima na tuweke msingi uliyo thabiti, nadhani inakuwa changamoto kubwa sana kama hatujaweza kuajiri walimu wa kutosha.

Hivyo basi, kwa sababu walimu hawatoshi kwenye shule za chekechea, tumepeana mwanya kwa wale wazazi ambao hawana uwezo watoto wao wasikose nafasi ya kujiendeleza kielimu. Mbona tusilipee hili nafasi ya kwanza kwamba tuajiri? Niliweza kuleta Hoja hapa nikasema uchunguzi wa uhaba wa waalimu wa chekechea katika Kaunti ya Kilifi na kuwe na mikakati ya mipangilio ya bajeti ya kuhakikisha kwamba tunaweza kupata nafasi ya kuajiri swala ambalo halijaweza kuzingatiwa kwa umakini.

Kwa hivyo, tukiwa hapa nitauliza, na ni vizuri kwamba Kamati husika imeweza kutoa mapendekezo ambayo yamejitokeza kinaganaga kwamba, la kwanza; kuwepo na Kamati ambazo zitakuwa zinaangalia usimamizi na utekelezaji wa ile miradi kule mashinani. Haijakuwa rahisi wakati tunaenda kuzindua mradi halafu tunakosa watu ambao watajumuisha ofisi na mradi kule

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mashinani. Kwa hivyo iwe ni moja ya yale maswala ambayo yatapewa nafasi ya kwanza, halafu ...

*(Hon. Kenga spoke off record)*

...utakosa watu ambao watakuwa wakijumuisha ofisi pamoja na mradi kule mashinani kwa hivyo iwe ni moja ya yale maswala ambayo yatapewa nafasi ya kwanza. Halafu ile miradi yote kama walivyosema kwa sasa tunaenda kutengeneza ile tunaita *supplementary budget* na wameuliza kwa sababu kwa ile *budget* kuu ambayo tuliweza kupitisha iligundulika kwamba kuna baadhi ya miradi ambayo tayari ilikuwa imeanza lakini pesa zao hazikuwekwa katika *budget* mheshimiwa Spika kwa sababu hiyo itakuwa vigumu hata kuitekeleza. Kwamba miradi yote ile ambayo ilikuwa tayari imeanza na ile ambayo ilikuwa haijaanza lakini ilikuwa ni miradi ambayo ilipendekezwa na ikaweza kupata nafasi ya *budget* zilizopita basi ipewe nafasi ya kwanza ili miradi ile iweze kutekelezwa. La msingi ni kuhakikisha kwamba miradi yote itatekelezwa ndani ya mwaka huu, mwaka wa fedha, ili mwananchi aweze kupata faida.

Kwa sasa, kumbuka kama alivyoongea Mwenyekiti ametueleza kwamba kuna miradi ya 2013/2014 ambayo haijakamilika. Gharama ya ujenzi miaka ile ni tofauti na gharama ya ujenzi miaka hii. Ingekamilika wakati ule tusingetumia pesa nyingi wala rasilimali nyingi kuweza kuziingiza kwa hiyo miradi. Jinsi tunavyochelewa kukamilisha hii miradi kwa wakati, tunapeana mwanya wa gharama ya ujenzi izidi kupanda na inafikia kiwango sasa hali inazidi kuwa mbaya.

Ningeuliza Kamati ya Utekelezaji kwamba ingewezekana mapendekezo haya ambayo yamejitokeza kwa Ripoti hii na Ripoti nyingine zozote zile, tuziwekee hata mda ambao kama ni baada ya miezi mitatu tunaangalia mapendekezo yetu idara wamefikisha wapi kuyatekeleza ili kwa mapema zaidi kama kuna ulegevu tuweze kujua na tuhakikishe kwamba tutaenda vizuri katika kuboresha huduma kwa jamii.

Mimi naamini kwamba tukiweka misingi iliyo thabiti katika maswala ya elimu, tutakomboa Kaunti yetu ya kilifi. Kama hilo halitafanyika tunaweza kufanya mengi sana ya kimaendeleo. Kama elimu itakuwa bado iko duni bila shaka tutakuwa tunapoteza. Tunahitaji elimu bora. Elimu bora haitapatikana bila kuzingatia na kuhakikisha tuko na walimu wa kutosha na tuko na sehemu ambazo ziko katika misingi mizuri ya kupeana hii elimu. Ndiyo watoto waweze kupata elimu bora na elimu hii tuitumie kukabiliana na umaskini na baa la njaa ambalo linasemekana kwamba kwa wakati fulani tunalazimika kutoa pesa za miradi kung'ang'ana na maswala ya njaa.

Mwaka huu mvua haikuwa ya kutosha kwa hivyo tayari tuko na njaa. Ina maana sasa pesa zote tutakuwa tunapata kutoka kwa serikali tuingize katika maswala ya njaa. Ni lazima tuwe na mikakati na mbinu za kuona kwamba ni vipi tunaweza kuthibiti hizi changamoto ambazo zinatupata. Zaidi miradi iweze kutekelezwa kikamilifu kwa wakati. Ninapongeza Mwenyekiti na pia ninapongeza moja ya yale mapendekezo ambayo yameweza kupeanwa hapa ni yale ambayo Kamati ya Elimu pia wameweza kupendekeza. Haya mapendekezo yameoana na yote ni ya kimsingi na yanapotekelezwa bila shaka tutafika pale tumelenga. Asanteni sana na naomba sote tuweze kuunga mkono. Asante.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Shukrani Mheshimiwa. Mheshimiwa Loice wakati ni wako sasa.

**Hon. (Ms.) Ngari:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia hii nafasi. Nikisimama hapa mimi ni Mwenyekiti mdogo wa Kamati hii ya utekelezaji. Kwanza natoa shukrani zangu kwa Mwenyekiti wangu mkakamavu pamoja na wanakamati wenzangu. Aliyoyasema mwenyekiti pamoja na wale walioweza kuchangia nayaunga mkono kwa dhati. Ni kweli kunayo

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

shida hasa upande wa hii Miradi. Sisi kama Kamati shida hii tulipo ulizana na waziri na maafisa wake tuliwawekea muda wa bada ya siku ishirini na moja (21) kuhakikisha kwamba shughuli hizi ambazo ziko mbele yao ambazo hazijafanyiwa kazi vizuri ziwe zimetekelezwa kikamilifu.

Tuko macho tukiona kwamba baada ya hizi siku tuone manufaa. Kama ni miradi iwe imetekelezwa na kama ni hao walimu wawe wameweza kuajiriwa kwa manufaa ya mkaazi wa Kilifi maana ni haki yake. Sisi kama wajumbe tukiwa tumepitisha kwamba miradi fulani ina haja ya kutekelezwa kwa muda fulani inastahili iwe hivyo.

Changamoto ambazo zinatukumba ambazo hata saa hii bado tuko na miradi ya tangu mwaka 2013 haijatekelezwa ni jambo la kuwarudisha nyuma wana Kilifi. Sisi kama Kamati ya utekelezaji tunataka kusema kwamba tunahakikisha miradi hii tunaisukuma kikamilifu ili iweze kutekelezwa iwe ya manufaa kwa jamii yetu ya watu wa kilifi.

Wajumbe wenzangu tungepitisha hii Hoja ambayo iko mbele yetu ndio tukaone kwamba miradi hii inatekelezwa ili iweze kufaidi watu wetu kwa wakati unaofaa. Kwa hayo machache, nasema asanteni. Naomba tupitisha Hoja ambayo iko mbele yetu .Asanteni sana.

**The Temporary Speaker** (Hon.Mumba): Nafikiri ikiwa nimekusikia vizuri umesema kwamba miradi itekelezwe katika siku ishirini na moja (21)?

**Hon.(Ms) Ngari:** Katika mapendekezo ambayo tuliandika wakati tukiandika hii Ripoti, kuna hii shule ya Kazameni ECD Centre; Mawesa Ward. Mheshimiwa Spika, tulipitisha kwamba bada ya siku 21 mradi huu uwe umetekelezwa. Nafikiri inajitokeza katika Ripoti yetu. Mheshimiwa Spika, ijapo leo wewe ndo unaongoza Bunge lakini pia wewe ni mmoja katika wanakamati wa Kamati hii. Labda ni vile hukuweza kuhudhuria wakati tukiandika hizi Ripoti.

*(Hon. Kenga stood on a Point of Information)*

**Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa wa Adu ako na habari kukujuza.Sijui kama unamruhusu aweze kukujuza?

*(Laughter)*

**Hon. (Ms.) Ngari:** Ooh sawa. Pole nilikuwa naongea na.....

**Hon. Kenga:** Thank you very much Mr. Speaker. If you look at part one of the recommendations of the implementation Report on ECD and issues of the caregivers and you go to item number three there is the 21 day period as she was saying. “The Department of Education and ICT formulate a policy and structure of monitoring and evaluation to be forwarded to the County Assembly for consideration and approval within 21 days upon receipt of this report.”

Mr. Speaker, when you move to item number five; “The Department of Education and ICT ensures that all County Government projects are branded for ease of identification within 21 days upon receipt of this Report failure to which the Department will be answerable to the oversight Committee.”

On item number nine “ The Department of ECD should ensure that all projects including Kadzameni ECD Centre in Mwawesa Ward which needed guard rails be fitted within 21 days upon receipt of this Report failure to which the Department will be answerable to the General Oversight Committee.” Thank you.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Asante. Natumai huo ndio ujumbe ulikuwa wataka kupitisha. Asante mheshimiwa Loice. Mjumbe wa Marafa naona ukinyosha mkono..

**Hon. Karisa:** Mheshimiwa Spika, mimi acha kwanza niweze kuomba waheshimiwa kupitisha hii Ripoti kwa sababu mwaka uliopita kulikuwa kuna kuajiriwa kwa hawa *caregivers*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

334 lakini kati ya wale kuna nane waliobaki. Hivi sasa wanania kuajiri walimu wa chekechea wasiopunguwa mia tatu na. Kwa hivyo nafikiri tukipitisha hii itakuwa kuna umuhimu tuweze kupata zile nyongeza wakajaze wale wanane kwanza halafu ndio waanze kuajiri wale wengine. Mimi naona kuna umuhimu sana wa hii Ripoti kupitishwa kwa sababu imetuletea hasara kwa kila mwaka.

Ukiangalia katika bajeti hii inayokuja, kama miradi hii ingemalizika yote, pesa zile ambazo tungepata kwa mwaka huu zingekuwa zinaangazia *project* nyingine mpya. Lakini pesa zile ambazo ziko haina budi zipungue kwanza kwa kumaliza miradi ile ambayo iko nyuma. Kwa hivyo, tunapopitisha Ripoti hii itakuwa bora zaidi kujikakamua kuona kwamba miradi hii inaisha kwa wakati unaofaa kusudi pesa tunazopata kila mwaka tuweze kutengeneza miradi ambayo inatunufaisha zaidi. Lengine mheshimiwa Spika tunaona kwamba miradi mingi wanakandarasi wanawacha hii miradi kwa sababu ya ucheleweshaji wa malipo. Na tunaona kwamba tunapopitisha hapa tunaweza kuwa na Kamati ambayo itatusaidia kule mashinani kuona kwamba miradi ikianza, mheshimiwa mhusika wa ile wadi anahusishwa na tena kuwe na Kamati ambayo itakuwa ina ufahamu. Badala ya kwamba serikali ya Gatuji la Kilifi inaweka mradi halafu mheshimiwa anashtukia kwamba maofisaa wako kule mashinani wanaenendelea na shughuli zao. Kwa hivyo, tunapopitisha hii kutakuwa kuna ule utaratibu ambao huo unaweza kusaidia wananchi wetu wakajua miradi ya Kaunti na itekelezwe kwa wakati unaofaa. Asante sana mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Member for Garashi. Kindly hand over the microphone.

**Hon. Ziro:** Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii ambayo umeweza kunipatia ili kuweza kupeana mchango wangu lakini kabla sijapeana mchango, kuna kitu ambacho kinanikera na mimi nataka nikizungumze. Kila mara tukija hapa saa zingine tunapata hii mitambo haifanyi kazi na kwangu mimi naona ni aibu kubwa sana. Kwa sababu kila wakati kuna watu ambao wanashughulikia hii mitambo lakini sasa shida ni kwamba ukifika mara unaambiwa laini ya mbele haifanyi kazi tumia laini ya nyuma. Tumekuja, laini ya nyuma mashini zote zimekufa. Sasa hii imekuwa ni shida na imekuwa ni donda sugu katika hili Bunge letu. Kwa hivyo, ninaomba kuwe na njia mwafaka ambayo itatumika ili hii mitambo irekebishwe tusiwe na haya mambo ya vipaza sauti kuzungushwa. Kwanza inatupotezea wakati halafu watu wakizunguka zunguka inakuwa shida kwa hiyo hilo liweze kuangaliwa.

Mimi nataka kuunga mkono hii Ripoti kwa sababu kuna mambo ambayo yanafanyika katika hiyo idara ya elimu ambayo hayapendezi. Ukiangalia katika Katiba ya nchi yetu ya Kenya kifungu cha kwanza na cha pili vina sema na naomba niweze kusoma kwa lugha ya kimombo. One:

“1. All sovereign powers belong to the people of Kenya and shall be exercised only in accordance with the Constitution”.

2. The people may exercise their power directly or through their democratically elected representatives”.

Tukiwa hapa tunawakilisha watu wetu kule chini. Tarehe tisa mwezi wa nne nilileta *Statement* ndani ya Bunge hili ya kuuliza kwa nini kuna miradi fulani ambayo imesimama katika Wadi ya Garashi. Tarehe kumi na sita (16) nikaletewa majibu ndani ya Bunge hili, na majibu hayo yalikuwa hayaridhishi kwa sababu kuna nakala ya *warning letter* ambayo

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*



iliandikwa tarehe kumi na tano (15) mwezi wa Aprili ambayo ni siku moja kabla ya majibu ama barua ya majibu kuandikwa.

Bunge hili wakati tulipojadili tukaona kwamba kuna vitu ambavyo vinaendelea katika hiyo *Department* na havifai. Tukaamua kwa kauli moja hapa kwamba anayesimamia Wizara ya Elimu yaani CEC aweze kuitwa ndani ya Bunge hili ili aeleze, ni kwa nini mambo kama haya yanafanyika. Lakini mheshimiwa Spika nakumbuka vizuri wakati tukifanya uamuzi huo ilikuwa ni tarehe 25 mwezi wa Juni mwaka huu saa nne na dakika tano ndani ya Bunge hili. Lakini mpaka leo hatujapata majibu yoyote kutoka kule Ofisi ya Elimu tukajuwe ni mambo gani ambayo yanaendelea.

Kwa hivyo, inaonekana ni kama kitengo hichi cha elimu kiko na utepetevu na kuna watu ambao wanalalia kazi yao. Kwa hivyo mheshimiwa Spika, Ripoti hii ambayo imeletwa hapa na hawa wanakamati wetu wazuri ambao walienda wakakaa wakadadisi maneno fulani mpaka wakaamua kuja na Ripoti hii. Tunawaunga mkono na pia ninaomba Bunge hili tuweze kushikana mikono na tuhakikishe kwamba wakati mwanakandarasi anapelekwa kule chini lazima mheshimiwa ambaye anasimamia ile wadi ajue.

Haya mambo ya kuenda uone mtu yuko kwa wadi yako na kazi inaendelea hujui hiyo kazi imeanza wapi inaenda mpaka ifikie wapi. Mtu amekaa pale ukimuuliza anakwambia enda ukaulize huko juu mimi nimetumwa kutoka ofisi ya Kilifi. Hayo mimi naona kama madharau na kama itaendelea hivyo basi itakuwa yale mamlaka ambayo wananchi wametupatia kuweza kuwa wakilisha katika Bunge hili, yatakuwa yanatukanwa na wewe ukiwa mmoja wao utatukanwa na mimi nitatukanwa. Leo hii naomba tuweze kukubaliana na Ripoti hii iende halafu tena haya mambo ya wanakandarasi kuenda chini kabla mheshimiwa mwenye hiyo wadi ajue iwe itakomeshwa. Kwa hayo machache na mengi nataka kusema naunga mkono Ripoti hii. Asante sana mheshimiwa Spika.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Asante mheshimiwa. Nataka twende Kakuyuni, *member for* Kakuyuni.

**Hon. Mramba:** Asante mheshimiwa Spika. Nami nasimama kuunga mkono Ripoti iliyoletwa mbele yetu nikisisitiza zaidi kwamba miradi iliyokwama iweze kumalizwa mara moja. Nikiwapatia mfano mmoja katika wadi ya Kakuyuni; kuna mradi ambao ulianza mwaka wa kifedha wa 2015/2016 mpaka waleo haujamalizwa. Ulijengwa lakini bado haujagongwa bati na kuwekwa milango na madirisha. Wanafunzi wanasoma chini ya mti hadi leo; tumejaribu kufwatilia tukaambiwa mwenye kandarasi aliwacha ule mradi. Walikuwa wanawake wanne wakakosana na kuwacha ule mradi. Miaka mitatu imepita kazi ya kufuta ile kandarasi kutoka kwa wale wanawake na kupewa mtu mwingine haijafanyika. Juzi ndio nimepeana gari langu watu wa works wakachukuliwa na kuletwa Kakuyuni ku *assess* na kutengeneza BQ; hadi leo haijapeanwa.

Sasa tunaona kwingine sio ulegevu wa mwanakandarasi bali ni afisi yenyewe. Naomba mkazo huu usiwe tu kwa wizara moja ya elimu bali iwe kwa wizara zote. Mradi ukianzishwa mwanakandarasi huwa anapewa kandarasi na kutia sainsi kwamba atamaliza ile kazi kwa kipindi cha muda fulani. Inakuwa vipi yeye ametia sainsi kwamba atafanya kazi kwa miezi sita halafu anaenda mradi unamaliza miaka mitatu hapo? Kuna ulegevu ni lazima tukaze kamba ili kwa afisaa yeyote ambaye ataonekana ana ulegevu afadhali aende nyumbani.

Hii miradi ya ECD ina umuhimu wake, kwenye katiba yetu ya Kenya ile *Fourth Schedule* inatupatia mamlaka ya kusimamia mambo ya ECD pamoja na *polytechnic*. Hata hii mambo ya kuweka pesa kwa *scholarship* ili kusomesha wanafunzi *Secondary school* ni kama kusaidia; kazi yetu hasa ni *nursery school*. Hivi karibuni nitaleta Mswada tupate fungu la *capitation*, kila

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mwanafunzi alipiwe shilingi elfu moja kwa mwaka, badala ya kuchukua pesa nyingi na kupeleka shule za sekondari, kama mwanafunzi hatapata *foundation* nzuri kule chini atafika vipi kule juu?

Hili jambo tumeliona katika kaunti nyingine na wamefaulu. Wewe mweyewe Bw. Spika tulienda sote mpaka Kakamega na tukaona wameshaanzisha *capitation*. Kila mwanafunzi anapata shilingi elfu moja kwa mwaka; kwa hivyo kama muko na wanafunzi 200 kwa mwaka wanapewa shilingi elfu 200, hizo zinagaramia vitabu na chaki. Hapo tukisema ni *free pre-primary education* itakuwa ni ya kweli. Lakini sasa fikiria, wanafunzi ni 100 walimu walioajiriwa ni wawili, hawawezi kutosheleza wanafunzi wote, inabidi 50 wafundishwe na walimu aliyeajiriwa na Kaunti na wale wengine wafundishwe na walimu wa wazazi. Hapo ni lazima watalipa karo, vile vile tumesaidia wapi?

Wacha tulipe hii *capitation* ili kuhakikisha kwamba ile *rate* inakuwa nzuri zaidi. Tumeona kuna uhaba wa walimu wa chekechea na hivi karibuni ile bodi iliyoondoka ilipokuwa inawaajiri kwa *permanent terms* walimu walio sasa, kuna wengine waliachishwa kazi kwa sababu hawakuwa na *TSC number*. Kwa mfano, kule kwangu kuna wawili waliachishwa kwa sababu hawana *TSC numbers*. La kushangaza mmoja analipwa mshahara mpaka leo ukienda Ganda kuna mmoja pia, aliachishwa kazi, hayuko shule hafundishi lakini kila mwezi anatoa pesa.

Haya maneno nishampelekea hata Katibu wa Kaunti na nikampa jina la huyo mwalimu. Unaweza sema ni huyo mmoja ama wawili kumbe ikawa wako kaunti nzima. Kuna baadhi ambao walielewana na mwenye kutayarisha mshahara, kwamba ukipata mshahara utachukua asilimia fulani nyingine nitumie. Naomba Kamati ya Elimu huo uchunguzi ufanyike mara moja. Inawezekana kwamba pesa nyingi zinaingia mifukoni mwa watu ambao hawastahili; kama aliachishwa kazi ilikuwa vipi mshahara unaenda kwa akaunti yake mpaka leo? Naomba huo uchunguzi...

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Kuna Hoja ya Nidhamu.

**Hon. Kenga:** Thank you very much hon. Speaker. The Member for Kakuyuni Ward is raising very grave issues where public funds are being misappropriated, if that will fit the explanation he is giving. I am a Member of the Education Committee and the Chairperson is present but we may not be in a position without your direction to pursue the matter. I am requesting that if the Member can submit further information, like the names of the people who are getting paid yet they are not working so that it can form a basis for us as Members of the Education Committee to pursue the matter.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you. I was going to give direction on the same. The Member for Kakuyuni the issue is very sensitive and you may not be in a position to submit the document now. I would urge that you liaise with the Committee on Education and the Chairperson is next to you, and a very close friend to you; you should have given him the information even before you submitted it to this House. I believe you will liaise with the Committee and take the necessary steps to address the matter.

**Hon. Mramba:** Most obliged.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Thank you. By doing so, you will be giving more work to the Chairperson on Implementation.

**Hon. Mramba:** Asante sana. Nitapeana majina ya wale wanaopokea mshahara mpaka leo na hawako kazini. Majina niko nayo nilishampa *County Secretary* sijui amefanya hatua gani lakini nitapatia Kamati majina hayo ili waweze kufwatilia jambo hilo. Tunaweza kusema ni wawili tu kumbe ni 100 kutoka wadi tofauti tofauti, pesa inaingia na kuna watu wanafaidika, hiyo sio haki. Tutilie mkazo zaidi jukumu letu la ECD.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Zaidi ya hivyo, namuunga mkono mwenzangu mheshimiwa Ziro kwamba hivi vifaa vilivyo hapa vilitumia pesa nyingi sana yamlipa ushuru na sioni kama zimetuletea dhamani ya pesa zilizotumika.

Kila mara ukiweka kadi haifanyi; unaambiwa uondoke uende mahali kwingine siku nyingine inakwama kabisa. Kwa nini tusielezwe kwamba hizi mashini hazifai? Ni afadhali tuweke kwa bajeti tununuliwe mashine nyingine. Itakuwa ni aibu; ile siku zili *fail* wakati tulikuwa tunaandika mkataba hapa na wale waingereza, *British High Commissioner* yuko hapa na mashini hazifanyi kazi, ni aibu gani hii.

Tunajivunia kwamba Bunge la Kilifi ndio lililojenga *Chamber* nzuri zaidi Kenya nzima lakini kumbe mitambo yake haifanyi kazi. Haitakuwa vyema, pesa nyingi zimetumika lakini tunavyoona mambo hayaendi sawa. Kama tutaambiwa hizi hazifai, ni afadhali tutenge pesa kwenye bajeti na tununue mashini nyingine ambazo ziko bora kuliko aibu hii tunayopata hapa mara kwa mara.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): I had seen a hand from the Minority Leader, the Member for Kambe Ribe.

**The Minority Leader** (Hon. Matsaki): Nimesimama kuunga mkono Ripoti iliyo mbele yetu. Wacha nipongeze Kamati iliyofanya kazi hii. Kusema kweli, hawakuenda Kilifi Kaunti nzima lakini zile walizoenda walipata haya majibu. Nataka niongezee kitu kidogo; mungeenda Kambe Ribe kuna miradi ya ECD kutoka mwaka wa pili tulipoingia hapa kipindi cha kwanza mpaka sasa tunavyozungumza haijamalizika. Kusema kweli, hii Wizara ya Elimu imezembea kumekuwa na ukora; hata hiyo Ripoti ambayo imetolewa sasa pia inafaa kufwatiliwa. Ukichunguza kuna mambo mengi kama Bunge tunayapitisha lakini kule upande mwingine kuna uhafifu na si ati hawajui kazi yao, lakini kwa sababu ya ule uchafu ambao umejificha pale ndio unakuta hali hazifanyiki.

Mimi ningeomba katika yale ambayo Kamati hii iligundua na ni muhimu hili Bunge litaheshimika ikiwa tutasimama na msimamo mmoja. Tuko hapa kama watu wa kufanya *oversight* upande ule mwingine. Kwa hivyo, mimi ningeomba hata wale ambao hawajazungumza ... na Bw. Spika ukiangalia wabunge hawa sioni kama kuna hata mmoja atakayesimama aseme anapinga ile Ripoti. Mimi ningeomba sote tuiptishe halafu iwe ni msukumo mmoja wa hii kazi ifanyike.

Bajeti ilifanywa tukaweka pesa na miradi haijamalizika; hatujui zile pesa zilienda wapi. Mfano wa mwaka wa fedha uliopita, mimi niliweka mradi na haya ni madarasa tu mawili ambayo bajeti yake ilikuwa shilingi milioni 5.5 na mpaka leo kazi ile haijapatiwa mwanakandarasi. Ukiuliza unaambiwa wataweka katika *supplementary budget*. Sasa zile pesa zenyewe ilienda wapi mpaka kufikia sasa hawajapeana hiyo kazi?

Hii Kamati ya *Implementation* inaenda sawa na Kamati ya Elimu. Kamati ya Elimu ina kazi kubwa sana kwa sababu uchafu wote uko pale. Hata ikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu yuko hapa ningeomba avute soksi juu, kwa sabbau yale madhara yanayofanyiwa hii Kamati ni makubwa zaidi. Kwa hivyo yakishagunduliwa pale watu wa *Implementation* inakuwa ni rahisi nao kuingilia.

Kwa hivyo, ningeomba Kamati zote mbili; jamani kila mmoja afanye majukumu yake. Kwa kweli kazi ni nyingi hata mara nyengine ukipata Kamati haishughuliki na haiendi kule wala kule pengine ni wale wenye viti wanajukumika kwengine. Kama mtu amejukumika sehemu nyengine ni vyema wale waliobaki waendeleo na zile kazi. Najua Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu ako kwenye Bajeti pia; Bajeti ina nyakati zake maalum. Kwa hivyo si rahisi kuwa

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

atakuwa na wakati mzuri sana kusema kuwa afanye kazi zake kikamilifu. Wakati hii Bajeti inaenda na nyakati, yeye naye ajue ile Kamati ambayo anaiongoza ni Kamati muhimu sana.

Tujipange na tuunge mkono Ripoti hii ili tuone haya matunda. Kwa hayo machache naunga mkono. Asante.

## COMMUNICATIONS FROM THE CHAIR

### CONSULTATION WITH LEADER OF MINORITY

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Mheshimiwa Mwenyekiti Kamati ya Elimu natumai leo unapokea kazi ya ziada maana kiongozi wa walio wachache pia amegusia mengi ambayo naamini mkishirikiana yataweza kuleta utendajikazi ulio sawa.

Pia nakuhimiza kwamba yale aliyoyanena uweze kushirikiana naye ili uhakikishe kila idara, hususan idara yako ambayo imesemekana ina uchafu na kiongozi wa wachache ataweza kukudokolea haswa ni uchafu wa aina gani ili katika utekelezaji na ukaguzi wa utendajikazi wa ile idara yako uwakilishe habari iliyo sahihi na kamili.

### COMPETENCE IN THE USE OF KISWAHILI DURING DEBATE

Waheshimiwa nataka niwaambie kwamba Kiswahili kitukuzwe. Tunapozungumzia lugha yetu tunaonekana kwamba tunatatizika mno maana tunaamua kuongea Kiswahili lakini maneno mengi yanayozungumzwa ni ya kizungu. Katika kanuni zetu za Bunge, zinatuhimiza tunapoongea katika lugha moja uweze kuenenda na lugha hiyo hadi tamati. Hii ina maana kwamba tutakapopata nafasi ya kuweza kupata mafunzo naona kama Bunge tutakuwa tunanufaika kuweza kujifunza lugha ambayo ni ya Kiswahili na itakuwa na manufaa kwetu. Kwa hivyo naamini kwamba hayo yakipangwa yatakuwa ya manufaa kwetu ili tujifunze lugha ya Kiswahili.

**Hon. Mramba:** Kwa kuongeza, hayo unayoongea hivi sasa ningependekeza tupangiwe kama siku saba za *training* na mwalimu mzuri wa Kiswahili aweze kutufundisha. Ni taabu kweli kwamba unaongea maneno mawili Kiswahili unaongeza la kiingereza. Ukiongea kidogo *Department*, hiyo *Department* ni Kiingereza sio Kiswahili. Kuna maneno fulani ambayo kama tunaweza pata wiki moja kule South Coast pale Jacaranda tunaweza kufundishwa kidogo angalau tukirudi hapa tukawa tunaongea Kiswahili sanifu.

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): Asante maana unayahakiki ninayoyazungumza maana hata katika kueleza hiyo hoja yako bado umetumia Kiingereza ndani. Kwa hivyo uhitaji upo na naamini kwamba Bunge litalishughulikia swala hili ili tuendeshe kazi yetu ya Bunge kwa nia inayostahili.

*(Question put and agreed to)*

## BILL

### *First Reading*

### PUNGUZA MIZIGO (CONSTITUTIONAL AMENDMENT) BILL, 2019

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Order for First Reading read - Read the First Time and ordered to be referred to the relevant Departmental Committee)*

### **COMMUNICATION FROM THE CHAIR**

#### MULTIMEDIA SYSTEM FAILURE

**The Temporary Speaker** (Hon. Mumba): There has been a concern on the system that we use for communication in this House and indeed it has been a long term issue that we have been experiencing. I will urge the administration of this Assembly to look into this issue so that we don't experience such embarrassments again in this House.

### **ADJOURNMENT**

In the absence of any other business in the Order Paper, I move to adjourn this House until today at 2.30 p.m.

**The House rose at 10:20 a.m.**

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*